

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



MKUTANO WA SABA

YATOKANAYO NA KIKAO CHA HAMSINI NA SITA

29 JUNI, 2017

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA HAMSINI NA SITA TAREHE 29 JUNI, 2017

Kikao cha Hamsini na Sita tarehe 29 Juni, 2017 Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi na Dua ilisomwa na Mhe. Spika.

I. PRESIDING OFFICER

Mhe. Job Y. Ndugai, Mb (Spika)

Makatibu mezani:

1. Ndg. Charles Mloka
2. Ndg. Laurance R. Makigi

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

WAZIRI MKUU

Hati ya Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa Mwaka 2015/2016 (*The Annual Report of Social Security Regulatory Authority for the Year 2015/2016*).

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO

Hati ya Uhamishaji Fedha Na. 1 ya Mwaka 2016/2017 (*Statement of Reallocation Warrant No. 1 of 2016/2017*).

Hati ya Uhamishaji Fedha Na. 2 ya Mwaka 2016/2017 (*Statement of Reallocation Warrant No. 2 of 2016/2017*).

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

1. Mhe. Omary Tebweta Mgumba - CCM
2. Mhe. Flatey Gregory Massay - CCM
3. Mhe. Martha Moses Mlata - CCM
4. Mhe. Ritta Enespher Kabati - CCM

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Swali Na. 462: Mhe. Njalu Daudi Silanga

Nyongeza: Mhe. Njalu Daudi Silanga
Mhe. Mariam Salum Msabaha

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA)

Swali Na. 463: Mhe. Joseph Michael Mkundi

Nyongeza: Mhe. Joseph Michael Mkundi
Mhe. Martha Jachi Umbulla

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Swali Na. 464: Mhe. Muhammed Amour Muhammed

Nyongeza: Mhe. Muhammed Amour Muhammed
Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara
Mhe. James Francis Mbatia

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Swali Na. 465: Mhe. Faida Mohammed Bakar

Nyongeza: Mhe. Faida Mohammed Bakar
Mhe. Rhoda Edward Kunchela
Mhe. Goodluck Araph Mlinga

WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

Swali Na. 466: Mhe. Mariam Nassoro Kisangi

Nyongeza: Mhe. Mariam Nassoro Kisangi
Mhe. Zainab Matitu Vullu
Mhe. Ruth Masereleli

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

Swali Na. 467: Mhe. Taska Restituta Mbogo

Nyongeza: Mhe. Taska Restituta Mbogo
Mhe. John John Mnyika

V. MATANGAZO

Mhe. Spika aliwatambulisha kwa Wabunge wageni mbalimbali waliohudhuria Bungeni, wageni 23 wa Mhe. Naibu Spika, wageni 35 wa Mhe. Anthony Mavunde, wageni 9 wa Mhe. Joseph Genzabuke, Wageni 6 wa Mhe. James Mbatia, wageni 30 wa Mhe. Seif Gulamali na wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Aidha, Mhe. Spika alitoa maelezo kuhusu kuongezwa kwa Shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatano tarehe 5 Julai, 2017 ili kufanya kazi ya kujadili na kupitisha Miswada 3 iliyoletwala kwa Hati ya Dharura.

VI. MIONGOZO YA SPIKA

Baadhi ya Wabunge waliomba Mwongozo wa Spika kama ifuatavyo:-

- Mhe. Pauline Gekul aliyeomba mwongozo kuhusu swali la Mhe. Rita Kabati kwa Waziri Mkuu ambaye alisisitiza kwamba kama alivyotoa Tamko la Serikali katika Sherehe ya Idd Mjini Moshi kuhusu kupiga marufuku usafirishaji wa mahindi nje ya nchi. Mhe. Pauline P. Gekul alitaka kujua mikakati ya Serikali kuhusu kununua mahindi kwa Wakulima kutockana na kupigwa marufuku hiyo, kwani wanaweza kupata hasara kama Serikali haitakuwa na mikakati ya kununua.

Mhe. Spika alitoa Mwongozo kwamba Hoja hiyo ni nzuri hivyo Serikali ilazimike kutoa kauli kwa wakati muafaka utakapofika.

- Mhe. John Mnyika aliomba mMwongozo kuhusu Miswada 3 inayowasilishwa kwa Hati ya dDharura akitoa mfano katika mwaka 1997 Miswada kama hii iliwasilishwa kwa Hati ya Dharura na kupidishwa haraka haraka na ndio maana sasa tunapata matatizo hayo. Aliomba Miswada hii ya sasa ijadiliwe na Bunge katika Mkutano unaofuata ili kupata muda wa wadau na Wabunge wenyewe kupata muda wa kuchambua kwa kina.

Katika hili Mhe. Spika alimtaka Mhe. Jenista Mhagama kufafanua kwa kusoma Kanuni 80(4)(6) na zingine kuhusu masharti ya Miswada kuletwa kwa Hati ya Dharura na alidhihirishia Bunge kwamba masharti yote yamezingatiwa na hivyo Bunge lione manufaa makubwa kwa Taifa hivyo alishauri Bunge lijadili na kuchambua Miswada hiyo. Aidha, Mhe. Spika alisisitiza kwamba Wabunge tuendelee na mchakato wa kuchambua Miswada.

VII. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Miswada ifuatayo ilisomwa kwa mara ya kwanza kama ifuatavyo:-

Muswada wa Sheria ya Mapitio na majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi wa Mwaka, 2017 [*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-negotiation of Unconscionable Terms) Bill, 2017*].

Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili wa Mwaka, 2017 [*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Bill, 2017*].

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka, 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2017*].

VIII. HOJA ZA SERIKALI

MAAZIMIO

Maazimio yafuatayo yaliwasilishwa na Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais.

- Azimio la Bunge Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Nairobi wa Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi (*Amended Convention for the Protection, Management and Development of Marine and Coastal Environment of the Western Indian Ocean*).
- Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi kutokana na vyanzo na Shughuli zinazofanyika Nchi Kavu (*Protocol for the Protection of the Marine and Coastal Environment of the Western Indian Ocean from Land-Based Sources and Activities*).
- Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Nagoya ya Kusimamia Upatikanaji na Mgawanyo Sahihi wa Faida zitokanazo na Matumizi ya Rasilimali za Kijenetiki (*Nagoya Protocol on Access to Genetic Resources and the Fair and Equitable Sharing of Benefits Arising from their Utilization to the Convention on Biological Diversity*).

Baada ya Waziri kuwasilisha hoja ya Maazimio hayo Mwenyekiti alimuita Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuwasilisha Maoni ya Kamati Mhe. Stanslaus Nyongo kuhusu Maazimio yaliyowasilishwa na Waziri kama yalivyo hapo juu.

- Mwenyekiti pia alimwita Mhe. Dkt. Imaculata Sware kuwasilisha Maoni ya Kambi ya Upinzani kuwasilisha maoni yake kuhusu Maazimio hayo.

Baada ya kuwasilisha Maoni ya Kambi ya Upinzani Wabunge wafuatao walichangia Maazimio kama ifuatavyo:-

- | | | |
|----------------------------------|---|---------|
| 1. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau | - | CCM |
| 2. Mhe. Danstan Luka Kitandula | - | CCM |
| 3. Mhe. Zubeir Mohamed Kuchauka | - | CUF |
| 4. Mhe. Peter Simon Msigwa | - | CHADEMA |
| 5. Mhe. Saada Salum Mkuya | - | CCM |
| 6. Mhe. Maulid Said Mtulia | - | CUF |
| 7. Mhe. Godbless Jonathan Lema | - | CHADEMA |
| 8. Mhe. Steven Julius Masele | - | CCM |
| 9. Mhe. John John Mnyika | - | CHADEMA |
| 10. Mhe. Musukuma Joseph Kasheku | - | CCM |
| 11. Mhe. Luhaga Joelson Mpina | - | CCM |

Baada ya Wabunge kukamilisha kuchangia alimwita mtoa Hoja kuhitimisha Hoja yake na kuhojiwa na kuafiki.

IX. KUAHIRISHA BUNGE

Shughuli za Bunge ziliahirishwa saa 7:30 hadi kesho Ijumaa saa 3:00 asubuhi tarehe 30 Juni, 2017.